

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



## TAARIFA KWA UMMA

### KUTHIBITISHA UDAHILI KWA WAOMBAJI WALIOCHAGULIWA NA CHUO ZAIDI YA KIMOJA

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inautangazia umma kuwa dirisha la kuthibitisha udahili kwa waombaji waliochaguliwa na chuo zaidi ya kimoja litakuwa wazi kuanzia tarehe **14/10/2018** hadi tarehe **20/10/2018**. Hivyo, waombaji wote waliochaguliwa na chuo zaidi ya kimoja kwa awamu ya tatu na ambao hawakuweza kujithibitisha katika awamu ya kwanza na ya pili watumie namba maalum "confirmation codes" zilizotumwa kwenye simu zao walizotumia wakati wanatuma maombi vyuoni ili waweze kujithibitisha kwenye vyuo wanavyovipenda.

[kuona majina ya waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja bonyeza hapa:](#)

#### **Waombaji wanana takiwa kufuata utaratibu ufuatao ili kujithibitisha:**

- a) Kunakili namba maalumu (special code) iliyotumwa kwa njia ya ujumbe mfupi kwenye simu yake;
- b) Kuingia katika akaunti yake iliyo katika mfumo wa udahili wa chuo anachokipenda kati ya vile alivyo chaguliwa; na
- c) Kuingiza namba hiyo maalumu katika mfumo wa udahili wa chuo anachokipenda ili kuthibitisha udahili wake katika chuo husika.

**NB:** Tume inapenda kusisitiza kuwa, mwombaji anatakiwa kuthibitisha udahili wake ndani ya muda uliopangwa. Aidha, Tume inaviarifu vyuo vyote kuwa mifumo yao iwe wazi ili kuruhusu waombaji kujithibitisha. Pia, waombaji wanakumbushwa kuwa matatizo yote yanayohusiana na namba maalumu "codes" yari potiwe kwenye vyuo husika kwa utatuzi wa haraka zaidi.

**Imetolewa na:**

**Katibu Mtendaji**

**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**14/10/2018.**